**WAPAGANI WATASEMAUONGO ILI KUENEZA MAFUNDISHO LAO?**

Nadhani kichwa kingine cha habari ambacho ni kizuri kwa ajiili ya makala hii kingekuwa ni “Usiseme uongo.” Lakini uhalisia wa makala hii ni kwamba imekusudia hasa kuwalenga wapagani na utayari wao wa kusema uongo ili kueneza imani yao.Kwa kadri ya wakristo, sote tunafahamu ya kuwa ni makosa kusema uongo (angalau wakristo wanafahamu). Biblia inaweka wazi kuwa waongo wote wataenda motoni, Ufunuo 21:8. Huukumbuka wimbo wa watoto kutoka katika Ufunuo 21:8? Hasa mwishoni pale wimbo huo unapoonyesha kitakachowatokea milele na milele wale wanaosema uongo bila kutubu, “ungua, ungua, ungua, ungua,ungua, ungua.”

Ndiyo, Wakristo wana kiwango cha malengo!!! (kiukweli kila mtu atahukumiwa kwa kutumia kiwango hiki.) Ni neno la Mungu. Na neno la Mungu linatufundisha kuwa tunatakiwa kufanana na mfano wake, Warumi 8:29; 2 Wakorintho 3:18. Na kwa kuwa Mungu hasemi uongo, Hesabu 23:19. Basi wale wenzangu na mimi wanaojitahidi kufanana naye, hawasemi uongo! Hata kama mkristo yu katika nyakati za udhaifu,ambapo hudhani jema litatokana na kusema uongo, HATUSEMI UONGO, kwa sababu neno la Mungu linafundisha kwamba wale wafanyao maovu ili mema yatokane na ovu wataangamia, Warumi 3:8. Hivyo, hapana, Wakristo hawasemi uongo. Kwa sababu maisha ya mkristo huratibiwa na neno la Mungu. Na dhamiri zetu hazitatuacha tuseme uongo, hata kama tunadhani yapo mazuri yatakayotokana na huo uongo. Kwa sababu tuna lengo katika nia zetu, nasi hatuwezi kulifikia kwa kuwa waongo wanene!

Vipi kuhusu wapagani? Kwa kuwa wanaikana Biblia kama kiwango cha malengo. Kwa kuwa wanadhani uadilifu kutokea kwa kutumia kile wanachodai ni bora jema. Mpagani anaweza kusema uongo, na akasema uongo kwa dhamiri safi, endapo kuna zuri litakalotokana na huo uongo? Jibu ni ndiyo! Wapagani wengi wanaamini kuwa Ukristo na Biblia huleta madhara. Wengi wanasadiki kuwa watoto wanaharibiwa wazazi wao pale wanapowafundisha mausia ya Mungu. Na, leo mpagani wa ukweli, anayesadiki kuwa uadilifu huamriwa na dhana ya kwamba ikiwa matokeo yake yatakuwa ya jema bora, hataona taabu kusema uongo ili kueneza mafundisho yao. Hivyo, kwa mujibu wa wapagani, siyo makosa kuwa muongo mkubwa, kama kuna jema bora litakalotokana nao.

Kwa ajili ya “jema bora” mpagani haonekani kuwa amesema uongo kama waliamini kuwa kuua watu 10,000 kule Beaumont kungeokoa maisha ya watu wengine Marekani. Baadhi yenu mlioko Beaumont, ni vema, nimefurahi kuwafahamu. Mnaona, mngeuawa kwa ajili ya jema bora, na kwa wapagani hili lingekuwa jambo la adili na la kuhalalishwa. Vipi kuhusu ubakaji? Hivyo hivyo! Kama waliamini kuwa kwa kubaka wangewaokoa wengi, wangebaka! Najua kuwa jambo hili linatisha. Najua wapagani wengi wasingependa kubaka na kwa hiyo wasingebaka. Lakini tena, baadhi ya wapagani kama mwandishi Sam Harris wanaamini, “hakuna kabisa lililo la asili, kuliko kubaka.” Hivyo kwa wapagani wengi, endapo wangeona wako katika hatua ya kuleteleza jema bora kwa kumbaka mtu fulani, watakuwa kwenye mazingira ya kuwajibika kubaka, na hapo ingekuwa ni kosa kutobaka. Kwa maana ni jambo la “adili” na “la asili” kulifanya.

Kwa kusema haya yote…kwa kujua kuwa mpaganiwa ukweli ataweza kusema uongo, atabaka, na kuua kwa kile kinachoonekana ni mwanya wa kuleteleza jema bora; Hivi kila mtu ataaminije, kila anachosema mpagani leo juu ya mageuzi na upagani. Pale wanapoamini kwa nguvu kwamba inakubalika kusema uongo, kupindisha mambo ili wakupate, ili wakugeuzie kwenye kile wanachokiamini kuwa kitabu kilichojaa uongo, kitabu ambacho kimesababisha maumivu ya moyo kuliko jema lolote hapa duniani. Kwa imani yao ya uadilifu, wanalazimika kusema uongo ili kukuongoa!

Vipi kuhusu Uislamu? Wanaamini yale yale kama wapagani. Uislamu unakataza kusema uongo, lakini wakati huo huo, Uislamu unatoa sababu za kukubalika kusema uongo. Hebu angalia hiki kilichoandikwa na Afif A. Tabbarah, msomi wa kiislam, katika “dhamira ya uislamu” kwenye ukurasa 247, Tabbarah alisema: “si mara zote uongo ni mbaya, kiuhakika; kuna wakati ukisema uongo ni faida na bora kiusalama kiujumla, na kwa ajili ya kuweka vizuri mazingira ya kuwasuluhisha watu, kuliko kusema ukweli. Katika hali hii, nabii anasema ‘Mtu ambaye anautumia uongo ili kuweka mazingira ya usuluhishi, hili huunga mkono mema au hutamka jema.” Hivyo, mimi kama mtu wanayenidhania kuwa kafiri, nitaaminije chochote wanachoniambia? Wasomi wa kiislamu,kwa mujibu wa Korani, wanapofundisha kwa uhakika kwamba kama ni manufaa kusema uongo, basi sema uongo! (Qur’an 16:106; 3:28; 2:225; 66:2)

Jamani, jihadharini, waalimu wa uongo husema uongo, 2 Wakorintho 11:3; Yeremia 14:4; 23:26; Warumi 16:18. Waislamu wameruhusiwa kusema uongo katika mazingira fulani endapo kuna masilahi yatakayotokana na kusema uongo. Nao wapagani, wanaamini kwamba itakuwa ni kosa kushindwa kusema uongo endapo ni "kitatokeleza chema bora kutokana na kusema uongo. Jihadharinini! Na kumbukeni kuwa inapotukia unasoma na kusikia kuhusu upagani na mageuzi (evolution). Wengi wao huamini kuwa kiuadilifu, ni jukumu kusema uongo ili wakushawishi kuamini kuwa wako sahihi.